

Wakurugenzi Watendaji

Wakurugenzi Watendaji wanajukumu la mwenendo wa uendeshaji wa kawaida wa Benki na wanatumia uwezo wote waliopewa na [Bodi za Magavana](#) kulingana na Articles of Agreement [Vifungo vya Maelewano]. Wakurugenzi Watendaji watano wanateuliwa na wanachama wenye idadi tano kubwa zaidi za hisa (kwa sasa ni: Marekani, Ujapani, Ujerumani, Ufaransa na Uingereza). Wakurugenzi Watendaji wengine wanachaguliwa na wanachama wengine. Katika IFC na IDA, Wakurugenzi Watendaji na Wapokezi wa Benki wanatumika kama Wakurugenzi Watendaji na Wapokezi rasmi wa IFC na IDA (kwa mda ambao nchi iliyowateuwa, ama yoyote kati ya nchi zilizowapigia kura, pia ni mwanachama wa IFC na IDA). Wanachama wa Bodi la Wakurugenzi wa MIGA wanapigiwa kura kivyao.

Kura za kawaida za Wakurugenzi Watendaji hufanywa kila miaka miwili, kawaida kwa mda wa Mikutano ya Mwaka ya Benki. Kwa miaka iliyopita, imekuwa desturi kwa sheria za uchaguzi kuhakikisha upana wa kigiografia pamoja na ustawi wa uwakilishi sambamba katika Bodi la Wakurugenzi Watendaji. Ongezoko katika idadi ya Wakurugenzi Watendaji waliopigiwa kura inahitaji uamuzi wa Bodi za Magavana kwa wingi wa asilimia 80 ya uwezo wote wa kura. Kabla Novemba 1, 1992, kulikuwa na Wakurugenzi Watendaji 22, 17 kati yao walikuwa wamechaguliwa kwa kura. Katika mwaka 1992, kwa sababu ya idadi kubwa ya wanachama wapya waliojuinga na Benki, idadi ya Wakurugenzi Watendaji waliopigiwa kura iliongezwa hadi kufikia 19. Viti biwili vipya, cha Urusi na mshiko mpya uliyozunguka Uswisi, uliongeza idadi mpya ya Wakurugenzi Watendaji kwa kiwango chake cha sasa cha 24.

Wakurugenzi Watendaji wanafanya kazi katika Benki kwa mihula yakuendelea na wanakutana mara nyingi kulingana na mahittaji ya shughuli za Benki. Wakurugenzi Watendaji wanashauriana na wanafanya uamuzi wa mikopo na mihakikisho ya IBRD na mikopo, karadha na mihakikisho ya IDA iliyofanywa na Raisi, na wanafanya uamuzi wa sera zinazo ongoza uendeshaji wa kawaida wa Benki. Wao pia wanajukumu la kupatia Bodi za Magavana, waraka za uhesabu, bajeti ya usimamizi, na ripoti ya mwaka ya upelekaji na sera za Benki na maswala mengine katika [Mikutano ya Mwaka](#). Katika shughuli za kuunda sera za Benki, Bodi la Wakurugenzi Watendaji hutilia maanani maoni yanayobadilika ya nchi wanachama kuhusu kazi ya Bank Group [Mshiko wa Benki] pamoja na ufahamu wa uendeshaji wa Benki. Mbali na kushiriki katika mikutano ya kawaida ya Bodi ya mara mbili kwa wiki, Wakurugenzi Watendaji pia hutumika katika kamati moja kati ya tano za kusimama: the Audit Committee [Kamati ya Uhesabu], Budget Committee on Development Effectiveness [Kamati ya Bajeti kwa Ufanisi wa Maendeleo], Personnel Committee [Kamati ya Wafanyikazi], na Committee on Governance and Executive Directors' Administrative Matters [Kamati ya Utawala na Maswala ya Usimamizi ya Wakurugenzi Watendaji]. Kamati husaidia Bodi ifanikishe wajibu wake wa juu kupitia ukaguzi wa ndani wa sera na mienendo.

Wakurugenzi Watendaji na Bodi

- ▶ [Wakurugenzi Watendaji na Wapokezi wa IBRD/IFC/IDA](#) (15K PDF) 
- ▶ [Wakurugenzi na Wapokezi wa MIGA](#) (15K PDF) 
- ▶ [Programu ya Kazi ya Bodi](#) Julai 2002 - Juni 2003 (35K PDF) 
- ▶ [Kalenda ya Bodi](#) Juni 2003 (10K PDF) 
- ▶ [Vifupisho vya Kalenda ya Bodi](#)

Uwezo wa Kura wa Nchi Wanachama

- ▶ [Kura na Kujiandikisha: IBRD](#)
- ▶ [Kura na Kujiandikisha: IFC](#)
- ▶ [Kura na Kujiandikisha: IDA](#)
- ▶ [Kura na Kujiandikisha: MIGA](#)

Uwezo wa Kura wa Wakurugenzi Watendaji

- ▶ [Hali ya Upigaji Kura ya Wakurugenzi Watendaji wa IBRD](#)
- ▶ [Hali ya Upigaji Kura ya Wakurugenzi wa IFC](#)
- ▶ [Hali ya Upigaji Kura ya Wakurugenzi Watendaji wa IDA](#)
- ▶ [Hali ya Upigaji Kura ya Wakurugenzi wa MIGA](#)